

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

Amami ya Simu "TAMISEMI" DODOMA
Simu Na: (026) 2322848, 2321607,
2322853, 2322420,
Nukushi: (026) 2322116, 2322146,
2321013

Barua pepe: ps@jmnoralg.go.tz
Unapojibu tafadhali taja -
Kumb. Na. CE.161/441/01'C/3



Tawala za Mikoa
na Serikali za Mitaa,
S. L. P. 1923,
DODOMA.

28.09.2015

Makatibu Tawala Mikoa,
TANZANIA BARA.

Yah: **AKAUNTI ZA VITUO VYA AFYA NA HOSPITALI ZA RUFAA
ZA MIKOA NA HOSPITALI ZA SERIKALI ZA MITAA**

Sera ya Afya inaelekeza vituo vya kutolea huduma za Afya kufungua akaunti ambazo zitatumika kutunzia fedha zitokanazo na gharama za kutoa huduma kwa wateja wa papo kwa papo (*Cost Sharing/User Fee*). Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na fedha za Mfuko wa Bima - NHIF

Kwa maana ya Sera na Miongozo ya Afya, Vituo vya kutolea huduma za afya ni pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Vituo vya Afya na Zahanati.

Kusudi la barua hii ni kusisitiza kwa Mamlaka zenu kufungua akaunti kwa ajili ya Hospitali za Rufaa za Mikoa na kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kufungua akaunti za Hospitali zao ili makusanyo yatokanayo na gharama za utoaji huduma, NHIF, fedha za papo kwa papo na Bima ya Afya ya Jamii (CHF/TIBA) zingizwe katika akaunti husika na zielekezwe katika uboreshaji wa utoaji huduma na uendeshaji hospitali na si vinginevyo.

Aidha, taarifa za ufuatiliaji na usimamizi elekezi kwa hospitali zenu zinaonyesha kudorora kwa huduma za Hospitali hizi kwa wateja na chanzo kikubwa kinatokana na usimamizi mbovu wa fedha zinazokusanywa katika hospitali hizi. Pia taarifa za Mkaguzi wa Nje zinaonyesha fedha hizi kutumika nje ya shughuli zinazolenga kuimarisha utoaji huduma.

Kwa barua hii, tunawaelekeza mfungue akaunti za Hospitali za Rufaa za Mikoa na zile za Mamlaka za Serikali za Mitaa na wale ambao tayari walishafungua akaunti hizi, waimarishe usimamizi wake na taarifa ya kila mwezi ya mapato na matumizi ya fedha hizi iletwe OWM-TAMISEMI. Aidha, katika kuimarisha utoaji huduma za Afya katika hospitali hizi, mnaagizwa kuleta taarifa za Mkaguzi wa Ndani kila robo mwaka kwa ajili ya mapato na matumizi ya fedha za hospitali zenu.

M. A. Pawaga
KAIMU KATIBU MKUU

(16)
RAS (17)